

# Mambo 50

**Mkenya anapaswa kujua kuhusu usimamizi wa fedha za umma kuambatana na katiba**


Commission for the Implementation of the Constitution
Utekelezaji wa katiba, jukumu la wote

IBP | KENYA
Open Budgets. Transform Lives.

# Utangulizi

Toleo hili limefanikishwa kwa ushirikiano kati ya tume ya utekelezaji wa katiba (CIC) na shirika la kimataifa la bajeti (International Budget Partnership - IBP).

## Tume ya Utekelezaji wa  katiba (CIC)

Tume ya kutekeleza katiba ilianzishwa chini ya sheria za katiba ya Kenya 2010, majukumu yakiwa ni pamoja na; kufuatilia na kuwezesha maendeleo, mabadiliko na utekelezaji wa sheria katika muda uliotengwa.

## Shirika la kimataifa la bajeti (IBP)

Shirika la kimataifa la bajeti hushirikiana na jamii ya mashirika yasio ya kiserikali kutathmini na kushinikiza bajeti za umma kwa malengo ya kupunguza umasikini na kuboresha huduma ya uongozi. Shirika hili la kimataifa la bajeti huelimisha viongozi na wananchi na kufanya utafiti wa uwajibikaji na uwazi wa fedha za umma nchini Kenya na duniani. Dkt. Jason Lakin ni afisa mkuu wa mipango na mtafiti mkuu aliye jijini Nairobi.

## Toleo hili

Toleo hili lina maelezo kuhusu usimamizi wa fedha za umma kuambatana na katiba na sheria ya kusimamia fedha za umma. Sheria ya kusimami fedha za umma iliundwa ili kuwezesha kuetekeleza Sura ya 12 ya katiba kuhusu usimamizi wa fedha za umma. Ni msimamo wa tume ya utekelezaji wa katiba (CIC ) kwamba ikiwa raia hawaelewi katiba na sheria ya fedha,itakuwa vigumu kuwashirikisha katika maswala ya fedha za umma,hali ambayo itaathiri haki yao ya kikatiba.

CIC itaendelea kufanya kazi na taasisi za uongozi za kitaifa na zisizo za kitaifa ili kuhakikisha malengo ya katiba yameafikiwa. Vilevile wanatoa shukurani kwa shirika la kimataifa la bajeti kwa kufanikisha uchapishaji wa toleo hili.

Twatoa shukurani kuu kwa shirika la Africa Centre for Open Governance (AfriCOG) kwa kufanikisha tafsiri ya toleo hili kutoka kwa lugha ya kimombo hadi kwa lugha ya kiswahili. Vilevile, tunamshukuru Isabella Mwagodi Kituri kwa kazi nzuri katika tafsiri ya toleo hili. Pia tunawashukuru Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA) na Drivers of Accountability Programme (DAP) kwa ufadhili wao. DAP ni mpango wa Department for International Development (DFID), CIDA and DANIDA.

*Nakala ya kiingereza ya toleo hili linaweza kupatikana katika wavuti wa CIC na IBP: www.cickenya.org or www.internationalbudget.org/kenya*

## Maelezo kuhusu mwongozo wa maswali na kanuni za toleo hili

Mwongozo wa maswali yanayoulizwa kila wakati na kanuni za toleo hili yanatoa mwongozo kwa umma kuhusu sheria ya kusimamia fedha za umma 2012. Mwongozo huu haufafanui sheria hizo kikamilifu, lakini huelezea sheria hii kuambatana na mahitaji ya umma wanaotaka kushiriki katika mchakato wa maamuzi kuhusu mapato na matumizi ya fedha katika serikali. Kwa sababu ya kuwepo kwa sheria mbalimbali zinazodhibiti matumizi ya fedha serikalini,tumetumia sheria zote husika kutayarisha mwongozo huu.

Mwongozo wa maswali na kanuni umetayarishwa kushughulikia maswali ya mtu wa kawaida kuhusu mchakato wa kutayarisha bajeti na usimamizi wa fedha. Maswali hayo yameangaziwa katika orodha ifuatayo baada ya utangulizi huu.

Kuna sehemu mbili muhimu zinazorahisisha matumizi ya mwongozo huu. Sehemu ya kwanza ni orodha ya tafsiri ya maneno. Sehemu ya pili muhimu ni orodha ya hatua za maandalizi ya bajeti ya kitaifa na katika kaunti katika sanduku nambari 1 katika sehemu ya mwisho ya mwongozo huu.

# Mambo 50 Mkenya anapaswa kujua kuhusu usimamizi wa fedha za umma kuambatana na katiba

## Orodha ya maelezo ya maswala na maswali

### Majukumu ya jumla ya raia katika matayarisho ya bajeti

1. Sheria ya kusimamia fedha za umma zinahusu nini na kwa nini nijali kuzifahamu?
2. Majukumu yangu ni yapi kuhusu jinsi serikali inavyotumia fedha za umma?
3. Je, kuna sheria inayoniwezesha mimi kama raia kushiriki katika harakati za bajeti?
4. Je, Naweza kushiriki tu kama mtu binafsi au naweza kushirikiana na makundi ya watu

### Ratiba ya maandalizi ya bajeti ya kitaifa

6. Nijitayarishe kushiriki katika maandalizi ya bajeti wakati gani?
7. Tunaweza kuisoma taarifa kuhusu sera za bajeti inapotangazwa, lakini nitashiriki kivipi kutoa maoni yangu wakati inapotayarishwa?
8. Ni wakati gani tunaweza kuona mapendekezo ya serikali kuhusu bajeti (Pamoja na maelezo ya makadirio) na kiwango cha fedha kilichotengewa sekta ya Elimu na afya?
9. Je, idara ya mahakama hutengeneza bajeti yao na kuituma bungeni?
10. Labda sikuelewa, lakini mapendekezo ya serikali kuhusu bajeti hutangazwa kwa umma wakati gani? Inasemekana kwamba lazima itumwe bungeni mwezi Aprili 30, lakini raia wataiona lini?

### Majukumu ya bunge katika matayarisho ya bajeti ya kitaifa

11. Kuna kiwango cha idadi ya mabadiliko tunayoweza kuomba bunge kutekelaza katika mapendekezo ya bajeti?
12. Je, kila mwaka kati ya mwezi Aprili 30 na Juni 30, bunge linaweza kufanyia mabadiliko mapendekezo ya bajeti, mradi tu wasisababishe upungufu wa fedha, na raia wanaweza kushiriki katika mjadala pamoja na wabunge wakati wowote katika muda uliotengwa? Kwa hivyo kuna muda wa kutosha wa miezi 2 siyo?
13. Je, kamati ya bunge kuhusu fedha na bajeti hupokea vipi maoni ya umma?
14. Nafahamu kwamba tangu kitambo, bajeti huidhinishwa kabla mwaka wa kifedha kuanza. Je, sheria ya kusimamia fedha za umma inatoa maelezo kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika muda huo

## Sera za bajeti ya kitaifa na utekelezaji

15. Kando na kushiriki katika kutayarisha bajeti, nimesikia kwamba wakenya wengine wameshiriki katika kufuatilia ikiwa fedha zimetumiwa kama zilivyopangiwa katika bajeti. Wengine wamefuatilia matumizi ya hazina ya fedha za maeneo bunge (CDF) . Je,sheria mpya zimetoa nafasi ya kufuatilia utekelzaji wa bajeti?
16. Tumezungumzia kuhusu umma kufuatilia matumizi ya bajeti. Kando na kutazama jinsi serikali ilivyotumia fedha ilizoahidi,kuna sheria zingine ambazo lazima serikali ifuate katika makadirio ya bajeti?
17. Nimesoma katika gazeti jinsi watu wanavyozozana kuhusu ikiwa deni la Kenya ni kubwa mno. Je,sheria ya kusimamia fedha za umma zinazungumzia kuhusu kiwango cha deni hilo au ikiwa lidhibitiwe kwa kiwango gani?
18. Naelewa kwamba serikali hulipa madeni ya mashirika ya kiserikali. Hii ni kumaanisha kwamba mashirika ya kiserikali huenda yakawa mzigo kwa watozwa ushuru. Je, sheria ya kusimamia fedha za umma huhakikisha kwamba raia wameelezwa kuhusu madeni haya?
19. Na misaada je? Kuna kiwango kinachokubalika cha msaada kinachoweza kupokewa na serikali, kama vile fedha kutoka kwa washirika wa miradi ya maendeleo?
20. Naelewa kwamba,mara kwa mara, hata kama serikali imepanga vyema bajeti, matukio ambayo hayakutarajiwa husababisha bajeti hiyo kubadilishwa. Je, sheria ya kusimamia fedha za umma zinaruhusu mabadiliko hayo?

## Serikali za ugatuzi na usambazaji wa fedha katika kaunti

21. Nilidhani tumeelekea katika utawala wa ugatuzi,lakini mmezungumzia tu kuhusu serikali ya kitaifa. Je kaunti?
22. Kuna hazina ya usawazishaji wa fedha ambayo hutoa fedha kwa kaunti. Inafanya kazi kivipi?
23. Nani anayeamua kiwango cha fedha kinachotolewa kwa kaunti?
24. Kaunti hupata fedha zao wakati gani?
25. Kuna masharti yeyote yanayoweza kuzuia serikali kutuma fedha kwa kaunti?
26. Ni wazi kwamba huenda serikali ya kitaifa na serikali za kaunti zikashirikiana mara kwa mara, kwa ajili ya kugawanya mapato ya fedha ya serikali. Je, sheria ya kusimamia fedha za umma inaelekeza jinsi serikali ya kitaifa na serikali za kaunti zitafanya kazi pamoja?

## Jinsi bajeti ya kaunti inavyoundwa

27. Nataka kujua kuhusu matayarisho ya bajeti ya kaunti na jinsi ninavyoweza kushiriki. Ndiyo sababu mlitueleza tutake kujua kuhusu sheria za kusimamia fedha za kitaifa. Basi nitashiriki kivipi na wakati gani katika matayarisho ya bajeti ya kaunti?
28. Lazima nitoe maoni kuhusu taarifa ya mpango wa maendeleo ya kaunti itakapochapishwa kila mwezi, lakini naweza kutoa maoni yangu wakati mpango huo wa maendeleo unapotayarishwa?

29. Hata kama nimeshiriki katika hatua ya kuandaa mipangilio, lakini ninaweza kushiririki kivipi wakati bajeti inapotayarishwa ili kuhakikisha makadirio yanashughulikia mahitaji yetu?
30. Kwa vile ni desturi kwamba taarifa ya mikakati ya kifedha huwasilishwa baada ya taarifa ya sera za bajeti ya kitaifa, hii inamaanisha pia mapendekezo ya bajeti ya kaunti yatawasilishwa baada ya mapendekezo ya bajeti ya kitaifa?
31. Katika ngazi ya kitaifa, kamati ya bajeti huwa na umuhimu mkuu kwa umma ambapo wao hupokea maoni yao. Kuna kamati ya bajeti katika bunge la kaunti?
32. Je, kuna masharti kuhusu mabadiliko yanayoweza kutekelezwa katika bunge la kaunti kama ilivyo katika bunge la kitaifa?
33. Je, kuna masharti yeyote kuhusu matumizi ya fedha katika serikali ya kaunti kama ilivyo katika serikali ya kitaifa?
34. Je, katika serikali ya kitaifa kuna mbinu zinazotumika kubadilisha bajeti baada ya kuidhinishwa,kama vile bajeti ya ziada na hazina ya dharura. Hizi zipo katika serikali ya kaunti?
35. 35. Katika serikali ya kitaifa, bunge linaweza kuidhinisha matumizi ya fedha hata kama mswada wa matumizi ya fedha haujapitishwa. Haya pia hufanywa katika serikali ya kaunti?
36. Sawa, na je kuhusu kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya kaunti?
37. Tulizungumzia kuhusu matakwa mapya kuhusu serikali ya kitaifa kuelezea jinsi inavyodhibiti deni la kitaifa na kulisimamia vilivyo. Na je, katika kaunti?
38. Je, serikali za kaunti zinaweza kupokea msaada kutoka kwa washiriki wa miradi ya maendeleo?

## Mapato na ushuru

39. Tumezungumza kuhusu matumizi ya fedha na madeni, na je, kuhusu ushuru? Sheria ya kusimamia fedha za umma zinasema nini kuhusu ushuru katika serikali ya kitaifa?
40. Je, sheria a kusimamia fedha za umma zinasema nini kuhusu ushuru wa kaunti?
41. Tumezungumzia kuhusu taarifa nyingi. Naweza kupata maelezo kuhusu taarifa zote zinazopaswa kuweka wazi kwa umma katika serikali ya kitaifa na ya kaunti na kwa wakati gani?

## Uwajibikaji

42. Hizi zote ni sheria nzuri lakini linalonitia wasiwasi ni uwajibikaji. Kenya imekuwa na sheria nzuri tangu jadi,lakini watu hupenda kuiba fedha za umma kila wanapopata nafasi. Sheria hizi mpya zimebuni njia ya kuhakikisha maafisa wamewajibika?
43. Ni nini kitakachofanywa ikiwa afisa mkuu wa fedha atashirikiana na waziri wa fedha kufuja fedha za umma? Nani atakayehakikisha wamewajibika?
44. Ripoti za mkaguzi wa kitaifa wa fedha zinazotathmini uwajibikaji wa taasisi za kiserikali huwasilishwa bungeni. Ripoti hizi hutolewa kwa umma?
45. Maafisa wa umma na taasisi za kiserikali watadhibitiwa kivipi wakifuja fedha?

## Miji, maeneo ya mijini,utoaji huduma na maswali ya ziada

46. Nimesikia kwamba miji na maeneo ya mjini wana mwongozo wa kutengeneza bajeti. Sheria ya kusimamia bajeti imeshughulikia swala hili?
47. Kuna mambo yeyote tunapaswa kufahamu katika sheria ya kusimamia fedha za umma,ambayo yanaweza kuathiri mapokezi ya huduma za elimu, afya na maji?
48. Huduma nyingi hutolewa na wahudumu wa kibinafsi kwa niaba ya serikali. Hali hii imechangia katika matumizi mabaya ya fedha. Sheria ya kusimamia fedha za umma imesema nini kuhusu maswala ya zabuni?
49. Kila kitu kipo katika sheria hii? Mbona sheria hiyo ni ndefu na mwongozo huu ni mfupi sana?
50. Stakabadhi husaidia, lakini kuna mtu yeyote ninayeweza kuzungumza naye ikiwa nina maswali ya ziada?

### 1. Sheria ya kusimamia fedha za umma zinahusu nini na kwanini nijali kuzifahamu?

Malumbano kuhusu jinsi rasilmali za umma zinavyogawanywa zikiwemo ardhi, huduma, fedha kama vile msaada wa masomo zina historia ndefu na wakenya sasa wanataka mabadiliko. Katiba ya mwaka 2010 imeleta sheria mpya inayoshinikiza usawa katika ugavi wa rasilmali utakaofaidi wakenya wote. Sheria hizi mpya zimetengenezwa kuzuia ubadhirifu na kuadhibu wanaofuja rasilimali za umma.

Sheria ya usimamizi wa fedha (PFM) imetoa sheria zinazoelekeza jinsi serikali ya kitaifa na serikali za kaunti zinaweza kupata fedha na mikakati ya kuzitumia. Sheria ya fedha za umma pamoja na katiba ya mwaka 2010, ndiyo kielelezo kikuu kinachomwelekeza rais, wabunge, magavana,

maseneta na wawakilishi wa kaunti,na mwananchi wa kawaida kuhusu majukumu yao katika maamuzi ya jinsi fedha za umma zinapaswa kutumiwa. Ikiwa unajali jinsi serikali inavyotumia fedha zako, na jinsi unavyoweza kushinikiza mkondo huo, basi itakuwa muhimu pia kufahamu sheria ya kusimamia fedha za umma.

### 2. Majukumu yangu ni yapi kuhusu jinsi serikali inavyotumia fedha za umma?

Tuna haki ya kujua jinsi serikali inavyotumia fedha zetu. Kumbuka fedha za umma ni fedha zetu,kwa sababu zimetokana na ushuru tunaolipa kama vile ushuru wa mapato, VAT na ushuru wa mauzo na bidhaa zinginezo tunazonunua kila siku. Fedha za umma pia zinajumuisha mikopo na misaada inayopokelewa na serikali kwa niaba ya mwananchi. Serikali haina fedha zake binafsi, fedha zote ni za raia wa Kenya na husimamiwa na serikali kwa niaba yetu.

Mbinu mwafaka zinazotumiwa na serikali kupata fedha na jinsi ya kuzitumia ni bajeti. Katika siku za awali, haikuwa rahisi kufahamau jinsi serikali inavyotumia fedha hizo.

### 3. Je, lakini kuna sheria inayoniwezesha mimi kama raia kushiriki katika harakati za bajeti?

Ndiyo tuanze na katiba. Katika sura ya 12 kuhusu maswala ya fedha, katiba inasema kwamba kutakuwepo uwazi, uwajibikaji pamoja na kushirikisha umma katika mchakato wa bajeti. Katiba inaelekeza kwamba mapendekezo ya bajeti ya kitaifa yawasilishwe bungeni kabla tarehe 30 Aprili. Kamati ya bunge kuhusu bajeti na fedha itafute maoni ya wananchi.

Hii inamaanisha kwamba kila mwaka mwezi Mei, una nafasi ya kuelezea bunge maoni yako kuhusu matumizi ya fedha ya serikali na mipango yake.

### 4. Je, nitashiriki tu kama mtu binafsi au naweza kushirikiana na makundi ya watu wengine?

Swali zuri. Ukweli ni kwamba ni vigumu kushinikiza maoni yako ukiwa wewe binafsi kutokana na sauti za wengine wengi wanaotaka majibu ya maswali mengine mengi. Ni vizuri kufanya kazi na makundi ya watu walio na maswali yanayoambatana na yako. Kwa mfano, shirika ambalo linashughulikia maswala ya walemavu na afya, na watawasilisha maswali yao bungeni. Ikiwa maswali yako yanaambatana na shirika hilo, unaweza kushirikiana nao uwape maoni yako wayajumuishe katika orodha yao. Mwaka uliopita, kamati ya bunge kuhusu fedha za umma, ilipokea maoni kutoka kwa mashirika kama vile muungano wa walimu KNUT, Shirika la kutetea maslahi ya watoto(the Child Welfare Society of Kenya) na kituo cha kutetea haki za kijamii na uchumi (Economic and Social Rights Centre). Yawezekana uungane na mashirika kama haya ili uweze kuwasilisha maoni yako, au kwa mashirika mengine yalio na maswali sawa na yako.

### 5. Je, haki ya kushiriki iko kwa pamoja katika katiba na katika sheria za kusimamia fedha za umma?

Sheria ya kusimamia fedha za umma inaelezea kwa kina zaidi ya katiba taratibu za kushirikisha umma. Raia wanaweza kutoa maoni yao kuhusu bajeti na kushirikiana na afisi ya bunge kuhusu bajeti kabla iwasilishwe bungeni. Ofisi hiyo pia ndiyo inayoshughulikia utafiti na kuelezea wabunge kuhusu bajeti. Raia wana haki ya kushiriki kuanzia hatua ya kwanza ya kuandaa bajeti, utekelezaji na ukaguzi wa bajeti.

### 6. Nijitayarishe kushiriki katika maandalizi ya bajeti wakati gani?

Sheria ya kusimamia fedha za umma hutoa nafasi kwa raia washiriki katika ngazi ya kitaifa na hata katika kaunti. Ushirika huu ni muhimu kwani kuna huduma ambazo hutumiwa mara kwa mara na umma kama vile elimu ambayo itashughulikiwa na serikali ya kitaifa. Maswala mengine kama afya yatashughulikiwa na serikali za kaunti.

Katika ngazi ya kitaifa sheria ya PFM hutaja tarehe maalum ambazo ni muhimu kukumbukwa. Ni muhimu kutazama kijisanduku nambari moja mwishoni mwa mwongozo huu wa maswali ili uweze kufahamu kalenda ya bajeti ya mwaka.

Ikiwa raia anataka kushiriki katika maswala ya bajeti, wakati unaofaa ni Februari Huu ndiyo wakati serikali hutoa taarifa ya sera za bajeti (BPS) bungeni.

Taarifa ya sera za bajeti ni taarifa inayotolewa na serikali kwa madhumuni ya kuelezea jinsi ya kupata fedha na matumizi yake katika mwaka wa kifedha na maswala yanayopewa kipau mbele. Taarifa hii siyo pendekezo lenye hesabu ya kina ya bajeti ya kila wizara. Taarifa hiyo inayojulikana kama mapendekezo ya bajeti au makadirio ya bajeti huletwa baadaye.

Sheria yaelezea wazi kwamba serikali itashirikisha maoni ya umma katika taarifa ya sera za bajeti. Hii inamaanisha kwamba kabla ya kila mwezi wa Februari serikali inapaswa kuwapatia nafasi mwananchi wa kawaida ili waweze kutoa maoni yao kuhusu maswala ambayo serikali itatilia maanani .Hatua hii inaambatana na matakwa ya katiba ya kushirikisha umma katika maswala ya kifedha Mwaka wa bajeti huanza mwezi Julai 1, ambapo taarifa hii inatarajiwa kuwa tayari katika miezi nne na nusu kabla kuanza kwa mwaka mwingine wa kifedha. Taarifa hiyo huwasilishwa bungeni tarehe 15 mwezi Februari, lakini inapaswa kutangaziwa umma kabla mwisho wa mwezi Februari. Pale taarifa hiyo ya sera za bajeti inapotangazwa raia wanapaswa kuisoma ili kufuatilia ikiwa serikali ilitilia maanani maswala waliyopendekeza.

Wizara ya fedha hutoa tangazo katika gazeti la serikali kati ya mwezi Februari na Machi la kuelezea raia washiriki katika kutoa maoni yao. Mwaka wa 2013 mwezi Februari 22, wizara ya fedha ilitangazia umma washiriki kwa kutoa maoni kupitia anuani ya barua pepe kufikia mwezi Machi 1 kwa anuani budget2013@treasury.go.ke. Raia wanaweza kushinikiza jinsi bajeti inavyopangwa kabla mapendekezo hayo kutangazwa rasmi bungeni mwezi Aprili.

### 7. Tunaweza kuisoma taarifa kuhusu sera za bajeti inapotangazwa, lakini nitashiriki kivipi kutoa maoni yangu wakati inapotayarishwa?

Serikali huandaa vikao na umma kwa kila sekta (kama vile elimu na afya) kabla ya kutoa taarifa ya sera za bajeti. Raia huuliza maswali na kutoa maoni katika vikao hivi. Serikali iliandaa vikao hivi mwaka 2011 na pia mwaka 2012/2013 na 2013/14. Vikao hivi ni kando na vikao vikuu vya kitaifa ambavyo kwa kawaida huandaliwa katika jumba la kimataifa la Kenyatta International Conference Centre (KICC) jijini Nairobi. Idara ya mahakama pia imeanza kuandaA vikao vya umma kabla kutoa mapendekezo yao ya bajeti[6].

Katika mkutadha huu, raia wanaweza kushinikiza taarifa ya sera za bajeti kwa kushiriki katika vikao hivi. Japo huenda ikawa vigumu kuuliza maswali na kutoa maoni kwa sababu ya jinsi vikao hivi vilivyoandaliwa, raia wanapaswa kuhamasishwa ili waweze kutumia vilivyo nafasi hizi.

Hizi ni nafasi tunazozifahamu zinazoandaliwa kupitia taarifa ya sera ya bajeti. Vilevile waziri wa fedha anapaswa kutoa tangazo kwa taasisi husika za serikali kabla mwezi Agosti 30, kuelezea jinsi umma wanavyoweza kushirikishwa katika matayarisho ya bajeti[7]. Tangazo hilo linaweza kujumuisha tarehe na ratiba ya vikao hivyo.

Hatimaye,sheria inadokeza kwamba kanuni zinaweza kuandikwa ili kutoa mwongozo kuhusu jinsi ya kushirikisha umma. Kwa mfano kanuni hizo zinaweza kuelezea hatua za kutangazia umma,pahali wanapoweza kutoa maoni yao kuhusu maswala ya kifedha, huku wakitilia maanani pia watu wasio na uwezo wa kusoma au kuandika, walemavu ,wanawake na makundi ya watu waliotengwa[8].

### 8. Je, tunaweza kupata mapendekezo ya kina ya bajeti ya serikali wakati gani (Makadirio ya bajeti) na viwango vya fedha vilivyotengewa sekta ya Elimu na afya?

Bunge linapaswa kujadili na kupitisha taarifa kuhusu sera za bajeti kufikia mwishoni mwa mwezi Februari. Kufikia mwezi Aprili 30, serikali inapaswa kutuma mapendekezo ya bajetibungeni. Wakati huohuo, bunge na idara ya mahakama lazima itume mapendekezo yake bungeni kufikia mwezi Aprili 30.

### 9. Kwa hivyo idara ya mahakama huandaa bajeti yake na kuituma bungeni?

Ndiyo. Bunge na idara ya mahakama hutayarisha bajeti zao kuambatana na katiba ya mwaka 2010 ,hatua ambayo ni tofauti na mienendo ya awali. Wizara ya fedha haishinikizi bajeti hizi, japo waziri wa fedha anaweza kutoa maoni yake kabla mwezi mei 15.

Marekebisho haya yalitekelezwa kuhakikisha kwamba bunge na idara ya mahakama zimejisimamia zenyewe tofauti na kuongozwa na wizara ya fedha.

### 10. Mapendekezo ya serikali kuhusu bajeti hutangazwa kwa umma wakati gani?

Sheria ya kusimamia fedha za umma inaelekeza kwamba makadirio ya bajeti yawekwe wazi kwa umma haraka iwezekanavyo baada ya kuwasilishwa bungeni[10]. Kufuatia kukosekana kwa tarehe maalum katika mwongozo huu, raia wanapaswa kushinikiza marekebisho yatakayowezesha kupokea mapendekezo ya bajeti wiki moja baada ya bunge kuipokea bajeti hiyo.

Marekebisho hayo ni muhimu kama ilivyonukuliwa katika katiba, kwamba kamati ya bunge kuhusu fedha inapaswa kuchukua maoni ya umma kabla kutoa mapendekezo yake, katika mwezi wa Mei. Lakini ikiwa umma hawajaona mapendekezo hayo ya bajeti,kama ilivyofanyika mwaka 2012 Mei, itakuwa vigumu kwa umma kushiriki. Raia lazima wasisitize kwamba ikiwa watashiriki kutoa maoni lazima wapewe taarifa za kina kwa wakati unaofaa.

### 11. Kuna kikomo cha idadi ya mabadiliko tunayoweza kuomba bunge kutekeleza katika mapendekezo ya bajeti?

Ndiyo. Unaweza tu kushinikiza bunge kufanya marekebisho yanayokubaliwa kisheria. Sheria ya kusimamia fedha za umma inadhibiti bunge kwa njia hii. Sheria ya fedha za umma inaelekeza kwamba ikiwa bunge linataka kuongeza mgao wa fedha kwa sekta ya Elimu, wapunguze fedha za sekta moja na kuzihamisha kwa Elimu. Hatua hii itazuia ongezeko la fedha zinazohitajika na upungufu katika bajeti. Bunge linaruhusiwa kupunguza matumizi ya fedha ili kukwepa kupungua kwa fedha[11].

Ikiwa bunge halijaridhishwa na matumizi ya jumla ya bajeti, mapato au upungufu inaweza kurekebisha haya yote kupitia mijadala na kurekebisha taarifa ya sera za bajeti. Hata hivyo, bunge limezuiliwa kufanya mabadiliko yatakayoongeza fedha kwa makadirio ya bajeti.

**12. Kila mwaka kati ya mwezi Aprili 30 na Juni 30, bunge linaweza kufanyia mabadiliko mapendekezo ya bajeti, mradi tu wasiongeze mapungufu ya fedha,na raia wanaweza kushiriki katika mjadala pamoja na wabunge wakati wowote katika muda uliotengwa? Kwa hivyo kuna muda wa kutosha wa miezi miwili, siyo?**

Ndiyo bunge linaweza kufanya marekebisho kadhaa lakini katiba imedhibiti uwezo wake kubadilisha mapendekezo ya bajeti.

Kumbuka kwamba kamati ya bunge kuhusu fedha lazima iwasilishe bajeti hiyo bungeni ili kuanzisha mjadala. Katiba inahitaji bunge kufanya marekebisho kuambatana na mapendekezo ya kamati ya bunge. Kamati ya bunge kuhusu fedha ikiwasilisha makadirio ya bajeti na bunge la kitaifa kuidhinisha kwa jumla, kuna mipaka ya kisheria inayozuia marekebisho yeyote.

Hali hii hupatia kamati ya bunge kuhusu fedha mamlaka yenye nguvu mno. Taswira hii inaashiria kwamba ni muhimu kushiriki katika awamu ya kutoa maoni kwa kamati ya bunge ya bajeti. Kamati hiyo husikiza maoni ya umma katika mwezi wa Mei (tazama sanduku nambari 1). Hii inamaanisha kwamba bunge halina miezi miwili ya kujadili mapendekezo ya bajeti ila mwezi mmoja pekee.

Baada ya kamati ya bunge kutoa ripoti yake, ripoti hiyo ndiyo huwa msingi wa mswada wa matumizi ya fedha. Mswada wa matumizi ya fedha ndiyo huidhinisha serikali kutumia fedha zilizoko kwenye mapendekezo ya bajeti. Bunge lazima lijadili na kuidhinisha msuada wa matumizi ya fedha,na kuufanya kuwa sheria ya matumizi ya fedha au bajeti iliyoidhinishwa.

Jambo la kutilia maanani ni kwamba mwezi mei kila mwaka ndiyo muhimu zaidi kwako wewe raia kushiriki katika kushinikiza mapendekezo ya bajeti wakati ambapo kamati ya bunge inatafuta maoni hayo. Ikiwa una maswala kuhusu sekta ya afya unaweza kuelekeza maswali na mapendekezo yako kwa kamati ya afya ambayo pia inawasilisha maoni hayo kwa kamati ya bunge ya fedha.

**13. Je, kamati ya bunge ya fedha za umma na bajeti hupokea kwa njia gani maoni ya umma?**

Mwaka wa 2012, kamati ya bunge ya bajeti ilifanya vikao katika kaunti 17. Mashirika yasio ya kiserikali na umma waliweza kutoa maoni yao kwa kamati hii. Kamati ya bunge ya bajeti iliwasilisha ripoti yake bungeni mwezi Juni 6. Kamati hii huenda ikafuata mkondo huu katika siku zijazo. Lakini raia wanaweza kufuatilia na kufahamu jinsi ya kushiriki kupitia ofisi inayosimamia maswala ya bajeti (tazama swali 50).

**14. Inafahamika kwamba, bajeti huidhinishwa kabla mwaka wa kifedha kuanza. Je, sheria ya kusimamia fedha za umma inatoa maelezo kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika muda huo?**

Jambo hili limekuwa tatizo mara kadhaa licha ya katiba kulidhibiti. Bajeti inapopitishwa nchini Kenya kupitia mswada wa matumizi ya fedha. Huu ni mswada unaoonyesha fedha zilizoidhinishwa na bunge kwa kila wizar, idara na mashirika,maarufu kama mfumo wa maamuzi kuambatana na mahitaji muhimu. Pale bunge linapokamilisha marekebisho ya bajeti, waziri wa fedha huwasilisha mswada wa matumizi ya fedha bungeni unaodhihirisha viwango vya fedha vitakvyotumika mwaka unaofuata. Mswada huo ukipitishwa hubadilika na kuwa sheria ya matumizi ya fedha unaoashiria bajeti kamili. Katiba inaelekeza kwamba ikiwa bunge halitakuwa limepitisha muswda huo kabla mwaka wa kifedha kuanza, basi bunge lina ruhusa ya kuidhinisha nusu ya kiwango cha fedha zilizokadiriwa katika mapendekezo ya bajeti zitumike kuendesha serikali ili kuzuia kutatiza shughuli zake.

Swala hili limesababisha watu kuenda mahakamani kushtaki serikali na bunge. Mahakama imetoa uamuzi kwamba hatua hii inaweza kutumika tu ikiwa mswada wa matumizi ya fedha umewasilishwa bungeni, lakini hauwezi kupitishwa katika muda unaotakikana. Hatua hii haiwezi kutekelzwa ikiwa wizara ya fedha haijawasilisha mswada huo bungeni.

Uamuzi huo ni muhimu kwani utadhibiti bunge ili liidhinishe tu matumizi ya fedha kuambatana na mabadiliko yaliowekwa katika mswada wa matumizi ya fedha. Ikiwa hakuna mswada basi inamaanisha kwamba mapendekezo hayo ni ya serikali tu. Ikiwa wizara itaruhusiwa kutumia fedha kuambatana na mapendekezo yake, wanaweza kuchelewesha mswada wa bajeti ili watumie mapendekezo yao bila kutilia maanani mapendekezo ya bunge. Raia wanapaswa kuwa macho kupinga tatizo hili.

**15. Kando na kushiriki katika kutayarisha bajeti, nimesikia kwamba wakenya wengine wameshiriki kufuatilia ikiwa fedha zimetumiwa kama zilivyopangiwa katika bajeti. Wengine wamefuatilia matumizi ya fedha za maeneo bunge (CDF). Je, sheria mpya zimetoa nafasi ya kufuatilia utekelezaji wa bajeti?**

Ndiyo. Raia wanaweza kufuatilia ikiwa fedha zilizotengwa katika bajeti zinatumika vilivyo. Sheria ya kusimamia fedha za umma inashinikiza serikali kutoa taarifa kwa umma kuhusu matumizi ya fedha ,na ikiwa yanaambatana na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka huo. (Tazama sanduku nambari 1 kuhusu kalenda ya bajeti)

Bajeti inapaswa kuchapishwa siku 21 baada ya kuidhinishwa na bunge. Kwasababu bajeti hupitishwa mwezi Juni 30, bajeti inaweza kutolewa mwezi Julai. Bajeti hii ndiyo nyaraka maalum inayoweza kutumiwa na raia yeyote yule kufuatilia matumizi ya fedha serikalini kuambatana na ahadi zao.

Mwaka mpya wa kifedha ukianza mwezi Julai 1, lazima kuwe na ripoti kuhusu matumizi ya fedha kila baada ya miezi mitatu. Ripoti hii itawezesha raia kufuatilia ikiwa fedha zilitumika vilivyo, kwa mfano iki-

wa fedha zilizotengewa hospitali zimetumika vilivyo.

Kila mwezi wa Novemba, serikali inapaswa kuchapisha taarifa kuhusu matumizi ya fedha. Taarifa hii hukagua matumizi ya fedha ya mwaka uliopita na kutofautisha na taarifa ya sera za matumizi ya fedha ili kuratibu kuambatana na uchumi wa kitaifa. Hatua hii huwezesha kukagua ikiwa serikali imeafikia malengo yake,ikiwa uchumi wa Kenya unaimarika na ikiwa kuna fedha za kutosha au zimepungua, za kutimiza malengo yaliopendekezwa na raia.

Sheria inaelekeza kwamba mdhibiti wa bajeti,cheo kipya kilichoundwa kuambatana na katiba mpya,lazima asimamie utekelezaji wa bajeti na kutoa taarifa kwa umma kitaifa na katika akunti kuhusu matumizi ya fedha za umma katika mwaka wa kifedha. Mdhibiti wa bajeti anapaswa pia kuzuia serikali kutumia fedha hizo vibaya au kuzifuja.

Ripoti zingine za matumizi ya fedha ambazo umma wanaweza kufuatilia, ni zile ripoti za kabla ya uchaguzi na baada ya uchaguzi. Ripot hizi zinapaswa kutolewa miezi minne baada ya uchaguzi mkuu na isipite zaidi ya miezi minne. Madhumuni ya kutolewa kwa ripoti hii ni

kuwezesha umma kuelewa jinsi fedha za uchaguzi ziliivyotumiwa na athari zake kwa uchumi wa taifa. Kwa mfano, ripoti hizi zijumuishe makadirio ya fedha zitakazotumiwa na tume ya uchaguzi na mipaka (IEBC) na ikiwa kulikuwa na ongezeko la maafisa wa polisi na usalama.

**16. Tumezungumzia kuhusu umma kufuatilia matumizi ya bajeti. Kando na kutazama jinsi serikali ilivyotumia fedha ilizoahidi, kuna sheria zengine ambazo lazima serikali ifuate katika makadirio ya bajeti?**

Ndiyo, Sheria ya kusimamia fedha za umma imetoa kanuni za kifedha zinazopaswa kutekelezwa. . Hizi ni pamoja na:

* Mtazamo wa matumizi ya fedha katika miaka mitatu hadi tano inapaswa kujumuisha asilimia 30 ya bajeti kutengewa miradi
* Kiwango cha fedha kinachoelekezwa kwa mishahara ya sekta ya watumishi wa umma (Kiwango maalum kinapaswa kuwekwa katika sheria)
* Na kati ya miaka mitatu na mitano ya matumizi ya fedha, mikopo inapaswa tu kutumika kwa miradi ya maendeleo.
* Deni la umma lidhibitiwe kwa viwango ambavyo serikali inaweza kumudu (Bunge liweke kiwango maalum kunachodhihirika kuwa rahisi kumudu)
* Viwango vya kutoza ushuru vifahamike wazi na visipande kiholela.

**17. Kuna maoni kwamba deni la Kenya liko juu mno. Je sheria ya kusimamia fedha za umma imezungumzia kuhusu deni la umma na litadhibitiwa kwa kiwango gani?**

Sheria ya umma inashinikiza serikali kutoa ripoti ya kila mwaka (Februari 15) kuhusu deni la umma na taarifa ya sera ya bajeti kwa wakati mmoja. Ripoti hii inatolewa kwa umma baada ya wiki mbili.

Kadhalika, serikali inapaswa kutoa ripoti kuhusu mikopo kila baada ya miezi minne,ili kuzuia watu kutanabahi mwishoni mwa mwaka kuhusu kile serikali inadaiwa na kiwango cha fedha kilicholipwa

Sheria pia imewezesha kuundwa kwa afisi ya kusimamia deni la umma ili kudhibiti mwenendo wa serikali katika kuchukua mikopo na kufuatilia gharama ya mikopo.Afisi hiyo pia hufanya utafiti kuhusu mikopo.

Msimamizi mkuu wa afisi hiyo huchaguliwa kupitia kanuni ya uwazi. Hiki siyo cheo cha kisiasa, japo msimamizi huyo atahudumu chini ya waziri wa fedha.

Kila mwaka kiwango cha mikopo lazima kiwekwe wazi katika taarifa ya sera ya bajeti na kuidhinishwa na bunge la kitaifa. Mikopo hiyo italipwa tu makadirio ya bajeti yalioidhinishwa na bunge. Kama ilivyonukuliwa katika swali la 16, kati ya miaka mitatu hadi mitano,matumizi ya fedha hizo za mikopo yatumike tu kwa miradi ya maendeleo.

### 18. Inasemekana kwamba serikali hulipa madeni ya mashirika ya kiserikali. Hii ni kumaanisha kwamba huenda jukumu la kulipa madeni ya mashirika hayo likawa jukumu la walipa ushuru. Je, sheria ya kusimamia fedha za umma huhakikisha kwamba raia wameelezwa kuhusu madeni haya?

Sheria haishinikizi mashirika ya kiserikali kutoa maelezo kuhusu shughuli zao. Ripoti ya ukaguzi wa matumizi lazima itolewe kila mwaka, miezi minne kabla mwaka kuisha. Ripoti hii itajumuisha maelezo kuhusu mikopo yeyote na ile ambayo serikali imesimamia.

Madeni ya mashirika ya serikali hayapaswi kulipwa na mtozwa ushuru, lakini iwapo mashirika haya yatashindwa kupata faida ,mtozwa ushuru atalazimika kulipa madeni yake. Ndiyo maana tunakushinikiza usome ripoti zao za kifedha kukagua ikiwa mashirika haya yanaimarika au yanapata hasara.

### 19. Na misaada je? Kuna kikomo katika kiwango cha msaada kinachoweza kupokewa na serikali, kama vile fedha kutoka kwa washirika wa miradi ya maendeleo?

Kiwango cha misaada kinadhibitiwa na waziri wa fedha ambaye huidhinisha misaada inayopokewa na taasisi za kitaifa za serikali. Sheria inaelekeza misaada hii ikaguliwe kupitia mbinu ya uhasibu ya kitaifa. Bunge limeelekezwa na sheria kuunda sheria zitakazosimamia misaada, na misaada hiyo

iambatane na mipangilio ya kimaendeleo ya kitaifa. Madhumuni ya sheria hii ni kuhakikisha taasisi za serikali hazipokei misaada ambayo haiambatani

na mipangilio ya miradi ya kimaendeleo ya serikali kama vile ruwaza ya 2030 au kurejelea mipangilio ambayo huenda ikawa inatekelezwa na taasisi zingine za kiserikali. Sheria huzuia taasisi

mbalimbali za serikali kutumia misaada na mikopo yeyeyote kabla bunge kuidhinisha au waziri wa fedha kutoa idhini kupitia kwa barua. Hatua hii inanuia kuzuia taasisi hizo kuanza miradi ambayo haijapangiwa na bunge.

**20. Mara kwa mara, hata kama serikali imepanga vyema bajeti,matukio ambayo hayakutarajiwa husababisha bajeti hiyo kubadilishwa. Je, sheria ya kusimamia fedha za umma zinaruhusu mabadiliko hayo?**

Kuna njia tatu ambazo serikali hutumia kukabiliana na mabadiliko katika bajeti. Mbinu ya kwanza wahasibu wanaruhusiwa kufanya marekebisho madogo katika bajeti zao kwa asilimia kumi. Wanaweza kuhamisha viwango vya fedha katika maeneo tofauti katika wizara yao, kwa kufanya maamuzi kuambatana na umuhimu wa swala linalowakabili. Hatua hii hutekelezwa pale inapoidhinishwa na wizara ya fedha bila kuipeleka katika bunge.

Kando na mabadiliko ya kawaida, katiba imeruhusu matumizi ya bajeti ya ziada iwapo bajeti halisi haitaweza kutosheleza mahitaji ya mipango yao. Bajeti hii ya ziada lazima iidhinishwe na bunge miezi miwili baada ya fedha kutumika kupitia mswada mpya wa makadirio ya bajeti ambayo hairuhusiwi kupita asilimia 10 ya bajeti ya jumla. Sheria hii inaweza kubatilishwa tu kupitia idhini ya bunge.

Hatimaye, ikiwa kuna mikasa,sheria ya kusimamia bajeti ya umma imeweka sheria ya kuunda hazina ya matumizi ya fedha ya dharura na ustawi wa maendeleo24.

Hazina hii hutumika kukabiliana na mikasa au shughuli ya dharura inayoathiri wakaazi na maslahi yao. Hazina ya fedha za dharura kila wakati inapaswa kuwa na shilingi billionni 10 ambazo zinaweza kutumika bila idhini ya bunge panapotokea mikasa.Hata hivyo, waziri wa fedha

lazima awasilishe ripoti kuelezea matumizi ya fedha hizo miezi miwili baada ya kutolewa, ili bunge iidhinishe hatua yake

**21. Tumeingia katika mfumo wa utawala wa ugatuzi, lakini mumezungumzia sana kuhusu serikali ya kitaifa. Je, kaunti?**

Serikali za kaunti zimeangaziwa katia sheria ya kusimamia fedha za umma. Kumbuka kwamba serikali za kaunti zinategemea njia mbili za kupata fedha, ya kutafuta faida kupitia mikakati yao kama kaunti na pia mapato kutoka serikali ya kitaifa. Mapato ya serikali ya kitaifa yanatakiwa kuwa kwa kiwango cha asilimia 15 ya mapato ya serikali ya kitaifa. Serikai za kaunti zinaweza kupokea misaada na mikopo kutoka kwa wafadhili. Lakini kufikia sasa mapato makuu ya kaunti yanatokana na serikali ya kitaifa.

Licha ya haya, serikali ya kaunti inapaswa kutafuta mapato yao wenyewe. Katiba inaashiria kwamba kaunti inaweza kuongeza mapato yake kupitia kutoza wakaazi wake ushuru au mali wanayomiliki, ushuru wa kujiburudisha na huduma wanazopokea. Ushuru wowote wa ziada lazima uidhinishwe

na bunge (Tazama swali 39). Katiba pia inatoa mamlaka kwa tume ya kitaifa ya kusimamia mgao wa mapato ya kitaifa (CRA) jukumu la kusaidia kaunti (na serikali ya kitaifa) kutafuta njia mpya za kuongeza mapato (Tazama swali 23 kuhusu CRA).

## 22. Kunayo hazina ya usawazishaji wa fedha ambayo hutoa fedha kwa kaunti. Inafanya kazi kivipi?

Katiba imewezesha kuundwa kwa hazina ya fedha za usawazishaji na ustawi wa maendeleo. Hazina hii hupokea nusu ya asilimia moja ya mapato ya serikali kila mwaka na hutumiwa kutoa huduma katika maeneo yanayokumbwa na umasikini. Hata hivyo, katiba inasema kwamba hazina hii inaweza kutumiwa moja kwa moja na serikali ya kitaifa au fedha zitolewe kwa kaunti kama mkopo au msaada. Ikiwa fedha hizo zitatolewa kama misaada kwa serikali ya kaunti basi itajumuishwa kama mapato yao. Hata hivyo, ikiwa fedha hizo zitatumiwa na serikali ya kitaifa,basi haitajumuishwa kama fedha za kaunti.

Kwa njia yeyote ile,bajeti hiyo itakuwa na shilling bilioni tatu kwa msingi ya makadirio ya bajeti ya mwaka 2010/11 au chini ya asilimia 2 ya jumla ya fedha zinazoelekezwa katika kaunti kuambatana na mapendekezo ya tume ya kitaifa ya kusimamia mgao wa fedha kuanzia mwaka 2012.

## 23. Nani anayeamua kiwango cha fedha kinachotolewa kwa kaunti?

Katiba imesema tume ya kitaifa ya kusimamia mgao wa mapato ya fedha CRA, lazima itayarishe mapendekezo ya mgao wa fedha utakaoelekezwa kwa serikali ya kitaifa na serikali za kaunti zitakazopokea fedha hizo kama kundi. CRA pia ina jukumu la kupendekeza jinsi fedha hizo zitakavyogawanywa kwa kaunti 47. Mapendekezo hayo yatafanywa kwa msingi wa ibara ya 203 katika katiba,na kuambatana na mahitaji ya maendelo ya kila kaunti.

Tume ya kitaifa ya CRA lazima iwasilishe mapendekezo ya miezi sita kabla mwaka wa kifedha kuanza (Januari), inaweza kubadilisha tarehe ikiwa wamesikizana na waziri wa fedha kufanya hivyo. Licha ya kwamba CRA hutoa mapendekezo kuhusu mgao wa fedha utakaotelekezwa kwa serikali za kaunti na kiwango kitakachopokewa na kila kaunti, bunge la kiatifa na la seneti ndiyo muamuzi wa mwisho. Kila baada ya miaka mitano, bunge la seneti na la kitaifa wataamua kuhusu mbinu ya kugawanya rasilmali katika kaunti.

Katika mwaka 2012, CRA ilipendekeza kwa bunge kupitisha utaratibu wa kugawanya fedha katika kaunti. Utaratibu huo unatazama maswala kadhaa yakiwemo, idadi ya watu katika kaunti (asilimia 45) viwango vya umasikini (asilimia 20) ukubwa wa ardhi (asilimia 8) majukumu ya kifedha ya kaunti ( asilimia 2) na mgao kwa kaunti zote (asilimia 25).Hata hivyo, utaratibu huu haumaanishi kwamba serikali za kaunti zitapokea mgao ulio sawa kwa miaka mitano. Kwa mfano, bunge lilikubaliana na CRA kwamba kaunti zipewe fedha kuambatana na idadi ya watu (Kama ilivyokuwa mwaka uliopita). Kaunti zinaweza kupokea fedha kuambatana na idadi ya watu kwa miaka 3 na kisha utaratibu huo kubadilika katika miaka 3 ijayo. Utaratibu huo utabadilishwa kila baada ya miaka 5. Hata hivyo, makadirio haya yanapaswa kuaangaziwa katika taarifa ya sera ya bajeti ya kitaifa (Februari 15).

Hatua hii inawezesha umma kujua kiwango cha fedha kitakachokuwa katika serikali ya kitaifa na jinsi kitakavyogawanywa katika wizara na taasisi mbalim-

bali. Miswada hii iidhinishwe siku kati ya 30 kutoka siku ilipowasilishwa bungeni.

## 24. Kaunti hupata fedha zao wakati gani?

Sheria imeelekeza kwamba fedha hizo zitumwe kila baada ya miezi mitatu na kabla ya tarehe 15 ya mwezi. Sheria pia imeelekeza fedha zinazotumiwa zichapishwe katika notisi ya gazeti ya serikali. Hatua hii ni muhimu, kutokana na historia ya ugatuzi, katika mataifa mengine fedha za kaunti hucheleweshwa mno na serikali ya kitaifa. Sheria imeelekeza ripoti hii ya mgao wa fedha itangazwe wazi ili umma wafuatilie ikiwa serikali inatimiza malengo yake. Sheria ya kusimamia fedha za kaunti pia im-eweka utaratibu wa kutatua matatizo ya kuchelew-eshwa kwa fedha (Tazama swali 26)

## 25. Kuna masharti yeyote yanayoweza kuzuia serikali kutuma fedha kwa kaunti?

Ndiyo. Serikali inaweza kuzuia kutoa fedha kwa serikali ya kaunti kufuatia sababu maalum kwa siku stini na kutoa tuu asilimia 50% ya bajeti yao. Bunge lazima liidhinishe mgao wa fedha kuzuiliwa kusambaza katika kaunti na kuandika upya idhini nyingine ikiwa siku sitini zitapita baada ya idhini ya kuwanza kutolewa.

Katiba imeelekeza kwamba serikali ya kitaifa inaweza kuzuia mgao wa fedha kwenda kwa serikali ya kaunti ikiwa kuna ukiukaji wa sheria. Sheria ya kusimamia fedha za umma imetaja baadhi ya makosa ya ukiukaji kama vile;

- Kaunti ikishindwa kulipa fedha
- Kushindwakutekelezamajukumuyakifedha
- Kuwa na upugufu kupita kiasi kilichoruhusiwa na sheria Maswaliyanayotokananaripotiyamkaguzi wa kitaifa wa maswala ya fedha au mdhibiti wa bajeti katika wizara ya fedha
- Matatizo yeyote yatakayo sababisha kaunti kushindwa kuendesha shughuli zake au kupata bidhaa na huduma

Fedha zinaposimamishwa kuelekea katika kaunti, waziri wa fedha atatakiwa kutafuta idhini kutoka kwa bunge katika siku 7 ili kusimamisha mgao. Bunge nalo lina siku 30 kuidhinisha hatua ya waziri wa fedha. Waziri wa fedha kisha atatakiwa kuandika taarifa ya kuwezesha kaunti kuendelea na shughuli zake akishirikiana na gavana ili kurekebisha makosa ya kifedha katika kaunti hiyo na kuwezesha kaunti kupokea tena mgao wa fedha katika ratiba ya muda ufaao.

## 26. Ni wazi kwamba huenda serikali ya kitaifa na za kaunti zikashirikiana mara kwa mara, kwa sababu ya kugawanya mapato ya fedha ya serikali. Je, sheria ya kusimamia fedha za umma inaelekeza jinsi serikali ya kitaifa na za kaunti zitafanya kazi pamoja?

Ndiyo. Sheria imewezesha kuundwa kwa baraza la ushirika wa kibajeti na baraza la kiuchumi kwa madhumuni hayo. Baraza hili hushirikisha maafisa wakuu wa kaunti wa fedha kutoka kaunti zote 47 na waziri wa fedha wa serikali ya kitaifa. Inajumuisha pia wawakilishi wa idara ya mahakama, na waziri mshirikishi wa taasisi za kiserikali. Baraza hilo hutumiwa kwa mawasiliano, majadiliano, kuhusu maswala ya bajeti, mgao wa mapato kati ya idara mbalimbali za seri-

kali. Baraza hilo hukutana mara mbili kwa mwaka na mwenyekiti wake ni naibu wa rais.

**27. Haya yote ni sawa,lakini nataka kujua kuhusu matayarisho ya bajeti ya kaunti na jinsi ninavyoweza kushiriki. Ndiyo sababu mulitueleza tutake kujua kuhusu sheria za kusimamia fedha za kitaifa. Basi nitashiriki kivipi na wakati gani katika matayarisho ya bajeti ya kaunti?**

Swali nzuri. Hakarati za bajeti zimefanana kwa njia nyingi kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti. Ukisoma ratiba ya nne ya katiba, utaelezewa kwa kina majukumu ya kaunti na serikali ya kitaifa,ili uweze kuelewa majukumu yao kuambatana na makadirio ya bajeti. Kwa mfano, Serikali ya kaunti haishughulikii elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu. Kaunti zinasimamia vituo vya matibabu na mauzo ya dawa. Utakapoelewa maswala gani yanashughulikiwa na kaunti utafahamu wakati ambapo unaweza kutoa maoni na kuuliza maswali kuhusu yale yanayokukera.

Lakini kabla kubuniwa kwa bajeti, lazima kuwepo mpango maalum. Bajeti ya kaunti huundwa kwa msingi wa mpango wa miradi ya maendeleo ya kaunti. Mpango huu huwasilishwa kwa bunge la kaunti tarehe 1 kila mwezi Septemba na kutolewa kwa umma siku saba baadaye. Mpangilio huo ndiyo msingi wa kuunda bajeti ya mwaka ujao.

Kaunti kadhaa zimeanza kuunda mipangilio ya mikakati na miongozo ya kushirikisha umma. Tafuta mpangilio huu ili uweze kushiriki katika kaunti yako. Ili kuona mfano, tazama mipangilio ya mikakati ya kaunti ya Machakos katika wavuti (http://www.kenyampya.com/userfiles/file/Machakos%20 Strategic%20Plan%20 Draft.pdf )

**28. Lazima nitoe maoni kuhusu taarifa ya mpango wa maendeleo ya kaunti itakapochapishwa mwezi Septemba, lakini naweza kutoa maoni yangu wakati mpango huo wa maendeleo unapotayarishwa?**

Ndiyo. Sheria imewezesha kuundwa kwa jukwaa la kaunti kuhusu bajeti na uchumi. Jukwaa hili la kaunti hujumuisha raia na maafisa wakuu wa kaunti na hujadili mipangilio ya maendeleo ya kaunti. Kadhalika, sheria huwezesha wanachama kuteuliwa kwa misingi ya kijinsia, walemavu na wataalamu. Hii ni nafasi nzuri kwa mashirika yasio ya kiserikali kutoa ushawishi wa nani atakayekuwa mwanachama katika jukwaa hili la kaunti kuhusu bajeti na uchumi.

Hata hivyo, sheria haitoi mwelekeo ulio wazi kuhusu jinsi jukwaa hili litakavyoendesha shughuli zake, mashirika yasio ya kiserikali na kijamii yameelezea hofu huenda gavana akatoa ushawishi kujumuisha marafiki zake. Ni jukumu lako wewe raia kuhakikisha jukwaa hili linatekeleza jukumu la kujadili maslahi ya umma katika kaunti.

Unaweza kusoma kwa kina kuhusu jukwaa hili katika wavuti; http://internationalbudget.org/wp-content/uploads/Joint-Brief-on-Participation- in-Kenyas-New-PFM-Law.pdf.

### 29. Hatakama tumeshiriki katika hatua ya kuandaa mipangilio, ninaweza kushiriki kivipi bajeti inapotengenezwa ili kuhakikisha makadirio yanashughulikia mahitaji yetu?

Harakati za bajeti ya kaunti huanza kwa hatua ya kutayarisha taarifa inayofanana na taarifa ya sera za bajeti (BPS) katika ngazi ya kitaifa (tazama swali Q6), lakini inajulikana kama taarifa ya mikakati ya kifedha (CFSP). Mikakati hii huwasilishwa kwa bunge la kaunti kila mwezi wa Februari 28.

Kumbuka taarifa ya sera za bajeti (BPS) huwasilishwa kila Februari katika bunge la kitaifa. Taarifa ya mikakati ya kifedha ya kaunti lazima itilie maanani taarifa ya sera za bajeti, kaunti wana wiki 2 kusoma BPS na kuandaa taarifa ya mikakati ya kifedha kuambatana na taarifa hiyo.

Sawiya na ngazi ya kitaifa, taarifa ya mikakati ya kifedha (CFSP) hutoa muongozo wa mipangilio ya mapato na matumizi ya fedha za kaunti kwa mwaka mmoja huku ikitilia maanani mipango ya miaka 2-3 ijayo. Kadhalika, itilie maanani maoni ya umma. Hii ndiyo hatua ya kwanza ambapo raia wanaweza kushiriki kwa kutoa maoni na kuuliza maswali, wanaweza kushiriki kupitia jukwaa la kaunti kuhusu bajeti na uchumi. (Tazama swali Q 24)

Pale wizara ya fedha ya kaunti itakapowasilisha taarifa ya mikakati ya kifedha (CFSP) kwa bunge la kaunti Februari 28, bunge hilo lina siku 7 kusambaza taarifa hii kwa umma. Bunge litaidhinisha taarifa ya CFSP katika siku 14. Nafasi hii itatoa wiki moja kwa umma kushiriki katika bunge kutoa maoni na kujadili maswala yanayowaathiri kabla bunge kupitisha.

Kumbuka taarifa hii ni nzito mno,maswala kama vile mpango wa kaunti wa matumizi ya fedha kwa uwekezaji kama vile barabara dhidi ya vivukio ni tofauti na malipo ya mishahara na huduma ni muhimu. Unaweza kuuliza swali pia kuhusu upungufu wa bajeti na ikiwa wataweza kujimudu katika mwaka huo wa kifedha. Katika ngazi ya kitaifa, sheria ya kusimamia fedha za umma hutoa mwongozo kwa maafisa wakuu wa fedha katika kaunti kutoa tangazo la jinsi umma wanavyoweza kushiriki katika kutayarisha bajeti ya kaunti. Tangazo hili lijumuishe tarehe za kushirikisha umma.

### 30. Kwa vile ni desturi kwamba taarifa ya mikakati ya kifedha huwasilishwa baada ya taarifa ya sera za bajeti ya kitaifa; je, mapendekezo ya bajeti ya kaunti yatawasilishwa baada ya mapendekezo ya bajeti ya kitaifa?

La hasha. Mapendekezo ya bajeti ya kitaifa yawasilishwe katika bunge la kaunti mwezi Aprili 30 kama ilivyo kwa mapendekezo ya bajeti ya kitaifa. Kadhalika iweke tarehe ambapo raia watashiriki. Hii inamaanisha kwamba afisa mkuu wa fedha katika kaunti ana muda mfupi wa kufanyia marekebisho mapendekezo ya bajeti na taarifa ya mikakati ya kifedha kabla kuziwasilisha. Inamaanisha pia bunge la kaunti lina siku 30 kujadili bajeti hiyo hadi tarehe 30 Juni. Vilevile wewe raia una muda wa kutosha kushiriki katika harakati hii.

Hata hivyo sheria inayosimamia fedha za umma haijadhihirisha wazi jukumu la kuwashirikisha umma katika maandalizi ya mapendekezo ya bajeti katika kaunti. Afisa mkuu wa fedha katika kaunti anapaswa

tu kuweka wazi ripoti hiyo kwa muda atakaoweza kufanya hivyo baada ya kuiwasilisha kwa serikali ya kaunti. Kwa hivyo ni jukumu la raia kushinikiza ripoti hiyo itolewe wiki moja kabla kuiwasilisha katika bunge la kaunti.

### 31. Katika ngazi ya kitaifa, kamati ya bajeti huwa na umuhimu mkuu kwa umma ambapo wao hupokea maoni yao. Kuna kamati ya bajeti katika bunge la kaunti?

Swali nzuri. Sheria ya kusimamia fedha za umma imeelekeza kuundwa kwa kamati ya bunge la kaunti kuhusu fedha ili iweze kukagua mapendekezo ya bajeti na kuiwasilisha katika bunge la kaunti. Tofauti iliyoko katika kamati ya kaunti na ile ya kitaifa bungeni ni kwamba ya kaunti haina msingi wa kisheria katika katiba. Hata hivyo, kamati ya kaunti inapaswa kukusanya maoni ya umma na hata kufanya vikao kama ilivyo katika kamati ya bunge la kitaifa kuhusu fedha.

Kwa sababu kigezo cha kuunda kamati ya bunge la kaunti kuhusu fedha hakikuangaziwa katika katiba, hawana mamlaka kama vile kamati ya bunge la kitaifa. Bunge la kitaifa linaweza kufanyia marekebisho mapendekezo ya bajeti yaliowasilishwa na kamati ya kaunti kuhusu fedha tofauti na bunge la kitaifa. Hata hivyo, kuna sheria ya serikali za kaunti ya kudhibiti mabadiliko yanayoweza kufanywa na bunge la kaunti kuambatana na mapendekezo ya kamati ya bunge kuhusu fedha katika kaunti.

### 32. Je, kuna masharti kuhusu mabadiliko yanayoweza kutekelezwa katika bunge la kaunti kama ilivyo katika bunge la kitaifa?

Ndiyo. Masharti yanafanana (Tazama swali 11). Bunge la kaunti linaweza kuongeza mgao wa fedha katika sekta moja ikiwa itapunguza mgao katika sekta nyengine ili wasiathiri makadiro ya bajeti yalivyopendekezwa na kuzuia upungufu zaidi katika bajeti.

### 33. Kuna masharti yeyote kuhusu matumizi ya fedha katika serikali ya kaunti kama ilivyo katika serikali ya kitaifa?

Ndiyo. Kuna kanuni za matumizi ya fedha zinazopaswa kufuatwa sawiya na katika serikali ya kitaifa.

Matumizi ya fedha ya kaunti hayapaswi kushinda kiwango cha mapato yao.

* Mtazamo wa matumizi ya fedha katika miaka mitatu hadi tano inapaswa kujumuisha asilimia 30% ya bajeti kutengewa miradi
* Kiwango cha fedha kinachoelekezwa kwa mishahara ya sekta ya watumishi wa umma katika kaunti (Kiwango maalum kinapaswa kuwekwa katika sheria)
* Na katika miaka mitatu na mitano ya matumizi ya fedha, mikopo inapaswa tu kutumika kwa miradi ya maendeleo.
* Deni la umma lidhibitiwe kwa viwango ambavyo serikali inaweza kumudu (Bunge liweke kiwango maalum kinachodhihirika kuwa rahisi kumudu)
* Viwango vya kutoza ushuru vifahamike wazi na visipande kiholela.

**34. Katika serikali ya kitaifa kuna mbinu zinazotumika kubadilisha bajeti baada ya kuidhinishwa, kama vile bajeti ya ziada na hazina ya dharura. Hizi zipo katika serikali ya kaunti?**

Serikali za kaunti zinapaswa kuanzisha hazina ya kaunti ya fedha za dharura sawa na hazina ya kitaifa ya fedha za dharura, na itumiwe tu kukabiliana na mikasa na maswala yanayoathiri raia na masilahi yao (tazama swali Q20). Malipo yanayotolewa kwa hazina hiyo ya dharura yasizidi asilimia 2 ya mapato ya mwaka uliopita. Malipo hayo yaidhinishwe katika miezi miwili baada ya kuwasilishwa kwa bunge la kaunti.

Kuna hatua pia za kuidhinisha bajeti ya ziada katika serikali ya kaunti, zinazofanana na hatua za serikali ya kitaifa. Ombi la kupata bajeti ya ziada linatakiwa lisipitishe asilimia 10 ya bajeti nzima ya mwaka huo ila tu ikiwa bunge la kaunti limeidhinisha hatua hiyo. Fedha hizo za hazina ya dharura ni lazima ziidhinishwe na bunge la kaunti miezi miwili baada ya kuzitumia. Sawiya na bunge la kitaifa, wahasibu wakuu wa kaunti, kwa idhini ya maafisa wakuu wa fedha katika kaunti,wanaweza kurekebisha matumizi ya fedha miongoni mwao kwa asilimia 10 kupitia "mfumo wa kufanyia maamuzi maswala muhimu yanayowakabili.

**35. Katika serikali ya kitaifa, bunge linaweza kuidhinisha matumizi ya fedha hata kama mswada wa matumizi ya fedha haujapitishwa. Haya pia hufanywa katika serikali ya kaunti?**

Ndiyo. Harakati imefanana na ile ya serikali ya kitaifa. Tazama swali Q14.

**36. Sawa, na je kuhusu kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya kaunti?**

Hatua hii ya kufuatilia utekezaji wa bajeti huanza na harakati ya kuidhinisha, kwa kutekeleza ahadi za serikali. Bajeti iliyoidhinishwa ndiyo msingi wa mswada wa bajeti unaotoa nafasi kwa bunge kupitisha sheria ya makadirio ya fedha ambayo huidhinishwa na bunge la kaunti na kutolewa  katika siku 21. Ikiwa haitachelewa itatolewa mwisho wa mwezi Julai.

Katika ngazi ya kitaifa, lazima ripoti za utekelezaji wa bajeti zitolewe kila baada ya miezi mitatu na kutolewa katika kaunti, bunge na umma kwa uwajibikaji na kufuatilia utekelezaji.

Kufikia mwezi Septemba 30 kila mwaka, ripoti hizi zinapaswa kutayarishwa na kutolewa mwezi mmoja baada ya mwisho wa mwezi wa tatu wa mwaka kwa bunge la kaunti na umma ili waweze kuikagua na kuifuatilia.

Mwezi Septemba 30 kila mwaka, (mwisho wa mwaka wa kifedha) wizara ya fedha ya kaunti wanapaswa kutoa taarifa yake ya kukagua bajeti kwa kamati ya kaunti kuhusu fedha na bajeti. Taarifa hii itaidhinishwa au kupitishwa na kamati hiyo katika siku 14 na kisha kuwasilishwa kwa bunge la kaunti. Bajeti

hiyo ichapishwe haraka iwezekanavyo. Taarifa hii ni muhimu kwa umma hasa kwa wale wanaotaka kushiriki kwa kuifuatilia au kufananisha na bajeti ya mwaka uliopita ili kubaini pale serikali imeshindwa kutekeleza mpangilio huo.

### 37. Tulizungumzia kuhusu matakwa mapya kuhusu serikali ya kitaifa kuelezea jinsi inavyodhibiti deni la kitaifa na kulisimamia vilivyo. Na je katika kaunti?

Matakwa katika ngazi ya kaunti ni sawa na yale ya serikali ya kitaifa.

Kwa mfano Februari 28, pamoja na taarifa ya mikakati ya kifedha, serikali ya kaunti inapaswa kuwasilisha taarifa kuhusu jinsi ya kudhibiti deni la umma kwa bunge la kaunti kila mwaka.

Katika mwaka huo, wizara ya fedha ya kaunti lazima itoe maelezo kila baada ya miezi mitatu kuhusu mikopo ya serikali ya kaunti kwa bunge la kaunti.

Tofauti na serikali ya kitaifa, katiba inadhibiti kiwango cha mikopo ambayo serikali ya kaunti inaweza kuchukua. Mikopo yote ya kaunti lazima isimamiwe na serikali ya kitaifa, serikali ya kaunti ikishindwa kulipa mikopo hiyo basi serikali ya kitaifa italipa kwa niaba ya serikali ya kaunti.

### 38. Je serikali za kaunti zinaweza kupokea msaada kutoka kwa washiriki wa miradi ya maendeleo?

Ndiyo zinaweza kupokea mikopo. Sheria za kuchukua mikopo katika serikali ya kitaifa ni zile zinazotumika katika serikali ya kaunti. Tofauti iliyopo ni kwamba lazima iidhinishwe na afisa mkuu wa fedha katika kaunti hiyo na wala siyo waziri wa fedha.

### 39. Tumezungumza kuhusu matumizi ya fedha na madeni, na je kuhusu ushuru? Sheria ya kusimamia fedha za umma inasema nini kuhusu ushuru katika serikali ya kitaifa na ya kaunti?

Sheria ya bajeti katika kaunti imeanzia katika katiba ambapo inaelezea ni ushuru wa aina gani unaweza kutozwa katika serikali ya kaunti. Katiba inaelezea kwamba serikali ya kitaifa inaweza kutoza ushuru wa mapato, ushuru wa bidhaa na kodi ya forodha.

Kaunti zinaruhusiwa kutoza tu ushuru wa bidhaa, huduma za kujiburudisha na ushuru ulioidhinishwa na bunge la kitaifa. Serikali zote za kaunti na kitaifa zinaweza kutoza ushuru kuambatana na huduma zinazotoa.

Katika sheria ya kitambo na ya sasa humu nchini Kenya, ushuru hushughulikiwa katika mswada wa fedha na wala sio mapendekezo ya bajeti. Mswada wa fedha ukiidhinishwa, huruhusu serikali kutoza ushuru na huwasilishwa bungeni mwezi Juni wakati mmoja kuambatana na ratiba ya bunge za Afrika Mashariki.

Kulingana na sheria, mswada wa fedha lazima uidhinishwe na bunge katika siku 90 zijazo baada ya mswada wa matumizi ya fedha kupitishwa.

Hii inamaanisha kwamba lazima upitishwe kufikia Septemba 30, ambapo ni siku 90 baada ya tarehe 30 Juni. Hii ndiyo siku ya mwisho ya kupitisha bajeti ya kila mwaka. Hata hivyo, kama tulivyojadili

awali,inawezekana kwa mswada wa matumizi ya fedha kucheleweshwa na kurejesha nyuma kalenda ya utekelezaji.

Kuna miezi mitatu ya kujadili ushuru katika bajeti baada ya bajeti kuidhinishwa na bunge. Hii ni nafasi nyingine ya kushirikisha umma watoe maoni yao. Sheria ya kusimamia fedha za umma inamshinikiza waziri wa fedha kutoa taarifa kuhusu mapato ya ushuru katika serikali na kuyaweka wazi kwa umma katika siku 21. Hatua hii huwezesha umma kufuatilia ikiwa serikali imeafikia malengo yake ya kupata ushuru au la.

**40. Sawa,hayo yanahusu ushuru wa kitaifa,na je, kuhusu ushuru wa kaunti?**

Utaratibu wa sheria ya kusimamia ushuru wa serikali umefanana hata katika kaunti. Kuna mswada wa fedha katika kaunti ambao huundwa pale maafisa wa kuu wa fedha wa kaunti watakapoitangaza . Mswada huo wa fedha lazima upitishwe katika siku 90 baada ya kuidhinsihwa kwa bajeti ya kaunti. Kalenda yake ya bajeti imefanana na ya kitaifa.

**41. Tumezungumzia kuhusu taarifa nyingi. Unaweza kunipa maelezo kuhusu taarifa zote zinazopaswa kusambazwa kwa umma katika serikali ya kitaifa na ya kaunti na kwa wakati gani?**

Ndiyo!

# Serikali ya kitaifa

Tume ya kitaifa ya mgao wa mapato CRA.

Kuwasilishwa kufikia January 1 kwa bunge la kaunti na kitaifa.

Taarifa ya sera za bajeti. Kuwasilishwa bungeni kufikia Februari 15. Kusambazwa kwa umma katika siku 15.

Taarifa ya mikakati ya kusimamia madeni ya serikali. Kuwasilishwa bungeni Aprili 30. Kusambazwa kwa bunge haraka iwezekanavyo.

Taarifa ya kukagua bajeti na mtazamo wa matumizi ya serikali. Huwasilishwa kwa waziri Septemba tarehe 30. Husambazwa kwa umma mwezi Novemba.

Ripoti ya kila baada ya miezi mitatu kuhusu bajeti ya kitaifa. isambazwe kwa umma katika siku 45 za mwisho wa miezi mitatu ya mwaka wa kifedha.

# Serikali ya kaunti

Taarifa ya mpangilio wa maendeleo ya kaunti. Kuwasilishwa kwa bunge la kaunti kufikia Septemba 1. Kusambazwa kwa umma katika siku 7 .

Taarifa kuhusu mikakati ya fedha ya kaunti. Kuwasilishwa katika bunge la kaunti kufikia Februari 28.

Mikakati ya kudhibiti madeni. Kuwasilishwa katika bunge la kaunti Februari 28 na kusambazwa kwa umma haraka iwezekanavyo.

Makadirio ya bajeti ya kaunti. Kuwasilishwa katika kaunti ya bunge kufikia Aprili 30. Kusambazwa kwa umma haraka iwezekanavyo.

Taarifa za kila baada ya miezi mitatu kuhusu utekelezaji wa bajeti. Kusambazwa kwa umma katika siku 30. Kusambazwa kwa umma siku thelathini kila baada ya miezi mitatu ya mwaka wa kifedha.

**42. Sawa, hizi zote ni sheria nzuri lakini linalonitia wasiwasi ni uwajibikaji. Kenya imekuwa na sheria nzuri tangu jadi, lakini watu hupenda "kuiba" fedha za umma kila wanapopata nafasi. Sheria hizi mpya zimebuni njia ya kuhakikisha maafisa wamewajibika?**

Ni kweli kwamba sheria husalia katika karatasi tu iwapo haitekelezwi. Lazima itekelezwe na serikali, ilindwe na idara ya mahakama,na kufuatiliwa na umma ili iwajibike.

Hata hivyo, sheria ya kusimamia fedha za kaunti imetoa majukumu na adhabu kwa serikali ya kaunti na kitaifa. Afisa mkuu aliye na jukumu la kusimamia fedha za umma ni mkaguzi mkuu wa fedha serikalini hata katika ngazi ya kitaifa na kaunti.

Afisa mkuu mkaguzi wa fedha huteuliwa rasmi na waziri wa fedha.

Maafisa wakaguzi wa fedha huteuliwa na afisa mkuu wa fedha wa kaunti.

Sheria yasema kwamba afisa mkuu mkaguzi wa fedha serikalini ana jukumu la kusimamia mipangilio ya bajeti na kutayarisha rekodi za maswala ya fedha. Wanapaswa kutumia fedha za umma kwa uwazi na uwajibikaji.

Sheria imemwelekeza afisa makuu wa kukagua fedha kumeleza waziri, mkuu wa sheria na spika wa bunge wa fedha kuhusu ufujaji wa fedha katika taasisi za serikali. Ikiwa maafisa hawa wote hawatachukua hatua mwafaka, mkaguzi wa fedha anaweza kuwasilisha malalamishi yake bungeni.

Madhumuni ya sheria hii ni kuhakikisha kwamba ikiwa fedha zinafujwa, mkaguzi mkuu ana uwezo wa kuwashtaki na kuwachukulia hatua kali. Mkaguzi wa fedha anahudumu chini ya waziri wa fedha.

**43. Sawa, na nini kitakachofanywa ikiwa afisa mkuu wa fedha atashirikiana na waziri wa fedha kufuja fedha za umma? Nani atakayehakikisha wamewajibika?**

Hakuna utaratatibu uliokosa matatizo. Ikiwa afisa wa mkuu wa fedha anashirikiana na waziri wa fedha kufuja fedha za umma, swali kuu ni umma watafahamishwa na nani kuhusu makosa yao? Taasisi zote za serikali zinapaswa kuwa na utaratibu wa kukagua stakabadhi za fedha ambapo wanaweza kugunduliwa iwapo wanalaghai wananchi. Ikiwa ukaguzi wa taasisi hiyo hautafaulu kudhihirisha ufujaji wa pesa, kuna mkaguzi wa fedha wa kitaifa (KENAO) kutoka nje ya taasisi anayeweza kuweka wazi maovu hayo. Maafisa wote wanosimamia fedha wanahitajika kutoa taarifa zao za fedha za umma kwa mkaguzi huyo wa kitaifa na mdhibti wa bajeti ambao watakagua ripoti hizo katika muda wa miezi mitatu ya kila mwaka wa kifedha. Mkaguzi wa kitaifa wa fedha atawasilisha ripoti hizo bungeni. ana jukumu la kuhakikisha fedha za umma zinatumika vilivyo katika serikali ya kaunti na ya kitaifa.

**44. Ulitaja kwamba ripoti za mkaguzi wa kitaifa wa fedha zinazotathmini uwajibikaji wa taasisi za kiserikali huwasilishwa bungeni. Ripoti hizi hutolewa kwa umma?**

Ndio. Taarifa zote za mkaguzi mkuu wa fedha kitaifa zinahitajika kusambaziwa umma. Kadhalika, un-

aweza kuzipata katika wavuti wa KENAO au uzipokee kutoka afisi yao. Awali vyombo vya habari na raia hawakuwa na haja na ripoti hizo, lakini sasa zina taarifa za kina zinazoweza kuwafungua raia macho kuhusu matumizi mabovu ya fedha za umma

### 45. Maafisa wa umma na taasisi za kiserikali wataadhibiwa kivipi wakifuja fedha za umma?

Ikiwa afisa wa kusimamia fedha atapatikana na makosa ya kufuja fedha za umma sheria ya kusimamia fedha za umma inapendekeza njia kadhaa za kumadhibu. Kipengee cha saba cha sheria hiyo kimetoa aina ya makosa katika sheria. ikiwa ni makosa ya matumizi mabovu ya afisi za umma, anaweza kufungwa kwa miaka miwili na faini ya shilingi million moja. Ikiwa ni ufujaji wa fedha, mshukiwa anaweza kufungwa kwa miaka mitano. Serikali pia inaweza kumpokonya mali yake kufidia ile aliyopora kutoka kwa serikali. Ikiwa ni taasisi ambayo imechukua mkopo bila idhini wataadhibiwa. Wanaweza kuzuiwa kuomba fedha kwa muda.

### 46. Nimesikia kwamba miji na maeneo ya mjini wana mwongozo wa kutengeneza bajeti. Sheria ya kusimamia bajeti imeshughulikia swala hili?

Ndiyo. Sheria imetoa mwongozo wa bajeti kwa maeneo ya miji. Kwa mfano, miji imeruhusiwa kutoza huduma wanazotoa na wanakubaliwa pia kutoza ushuru. Lakini wanapaswa kupokea mapato kutoka kwa kaunti zao. Sheria imeelekeza kwamba kaunti lazima ziwe na utaratibu kutathmini viwango vya huduma zinazohitajika katika maeneo ya miji wanapopanga mgao wa fedha katika maeneo ya miji. Utaratibu huu hujumuisha idadi ya watu, viwango vya umasikini,eneo na kadhalika. Utaratibu huu utahakikisha fedha zinazohitajika zimetolewa.

Miji pia inatarajiwa kupanga bajeti na mipangilio kwa njia inayofanana na taratibu za serikali ya kitaifa. Wanapaswa kufuata kanuni za makadirio ya fedha. Tofauti iliyopo ni kwamba mipangilio yao huidhinishwa na bodi ya miji. Ikiwa unataka kufahamu zaidi kuhusu taratibu hizi,soma sheria za maeneo ya miji 2011.

Afisa wa kusimamia fedha za maeneo ya miji na miji ana jukumu la kuhakikisha kwamba umma wanashirikishwa katika mipango ya maendeleo na bajeti katika kaunti zao. Afisa huyu huteuliwa na afisa mkuu wa fedha katika kaunti.

Maeneo ya miji na miji inadhibitiwa kisheria dhidi ya kuomba fedha kutoka kwa soko la hisa. Wanaweza kuchukua mikopo kutoka kwa kaunti au moja kwa moja kutoka kwa benki. Wanaweza pia kupokea misaada na mikopo iliyoidhinishwa na afisa mkuu wa fedha katika kaunti.

### 47. Kuna mambo yeyote tunapaswa kufahamu katika sheria ya kusimamia fedha za umma, ambayo yanaweza kuathiri mapokezi ya huduma za elimu,afya na maji?

Ndiyo, kazi ya kubaini jinsi huduma hizi zitakavyotolewa bado haijakamilika na sheria ya kusimamia fedha za umma haijabaini wazi kuhusu huduma hizo. Ni muhimu pia kudadisi shughuli za halmashauri ya

mpito na jinsi serikali inavyogawanya majukumu ambayo hayajaangaziwa katika katiba.

Hata hivyo, sheria ya kusimamia fedha za umma inaathiri zaidi sekta ya maji. Sababu ya tatizo hili ni kwamba maji husambazwa na bodi tofauti tofauti. Sheria ya kusimamia fedha za umma inaruhusu kaunti kutumia rasilmali na huduma zake kwa kuzisimamia. Hizi ni pamoja na huduma ya maji, ambayo sasa imeondolewa kutoka kwa kitengo cha serikali za wilaya na kuhamishwa kwa mashirika kutokana na usimamizi mbovu.

## 48. Huduma nyingi hutolewa na wahudumu wa kibinafsi kwa niaba ya serikali. Hali hii imechangia katika matumizi mabovu ya fedha. Sheria ya kusimamia fedha za umma imesema nini kuhusu maswala ya zabuni?

Sheria ya kusimamia fedha za umma haijazungumzia kwa kina kuhusu zabuni, japo imetajwa katika katiba. .Katiba inapendekeza sheria tofauti za zabuni na kuelekeza zabuni itolewe kwa haki, usawa, uwazi na kwa gharama isiyo ya ulaghai. Katiba imetoa adhabu kwa wanakandarasi ambao hawajatoa huduma bora au wamehusika katika ufisadi, wameshindwa kulipa ushuru na kukiuka kutoa ajira kwa usawa.

Utoaji zabuni hudhibitiwa na sheria ya kusimamia zabuni na mauzo (iliyoratibiwa 2010), ambayo ilibuni pia halmashauri ya kusimamia zabuni nchini Kenya. Sheria hii haijafanyiwa marekebisho tangu katiba kupitishwa. Kuna haja ya kufanya hivyo.

## 49. Kila kitu kipo katika sheria hii? Mbona sheria hiyo ni ndefu na mwongozo huu ni mfupi sana?

Hatujaangazia maswala yote. Tumedadisi yale maswala yalio muhimu zaidi kwa mwananchi. Lakini sheria imezungumzia maswala mengi kuhusu maswala ya kifedha, mikopo na kadhalika. Unaweza kusoma zaidi katika wavuti huu:

***http://internationalbudget.org/wp-content/ uploads/brief15.pdf or at www.cickenya.org***

Unaweza pia kusoma sheria ilikupata maelezo zaidi kuhusu maswali yalioangaziwa hapa. Unaweza kudadisi pia ripoti za maswala ya fedha kwa kufanya utafiti wa sheria za fedha ili kutazama ikiwa wanatoa taarifa zinazofaa.

Hatimaye, kumbuka kwamba kuna sheria zinazoundwa kuunga mkono sheria hii na zitajumuisha maelezo zaidi kuhusu maswala kadhaa na pia jinsi ya kushirikisha umma na kuwawezesha kupata maelezo zaidi.

## 50. Stakabadhi husaidia, lakini kuna mtu yeyote ninayeweza kuzungumza naye ikiwa nina maswali ya ziada?

Mashirika kadhaa hushughulikia maswala ya bajeti nchini Kenya. Lakini pahala pa kuanzia ni katika ofisi ya bajeti bungeni. Unaweza kusoma wavuti wao kupitia:

***http://www.parliament.go.ke/index.php?option=com_content&view=article&id=201:parliamentary-budget-ofice-pbo&catid=77: parliamentary-budget- ofice-pbo***

## Anuani yao ni:

Parliamentary Budget Ofice,
Protection House,
Gorofa ya 10 Parliament Road
Sanduku la posta 41842, 00100 – GPO, NAIROBI.
Simu: +254 - 020 - 2133074, 2221291-3 or 2848000
Barua pepe: **info@parliament.go.ke**

## Unaweza pia kuwasiliana na shirika la CIC na IBP kupitia anuani zifuatazo

Commission for the Implementation of the Constitution
Parklands Plaza,
Sanduku la posta 48041, Nairobi
Simu : 020 2323510
Barua pepe: **info@cickenya.org**

Au

International Budget Partnership
Sanduku la posta 19875 – 00202
Nairobi
Simu: +254729937158
Barua pepe: **lakin@cbpp.org**

## Ikiwa una maswali kuhusu matayarisho ya bajeti, unaweza kuwasiliana na taasisi ya kitafa ya uchumi IEA

Jumba la ACK Garden, gorofa ya 5, Block D,
1st Ngong Avenue, Upper Hill/Community,
Sanduku la posta 53989 00200,
NAIROBI, KENYA
Simu: (+254-20) 2717402, 2721262
Barua pepe: **admin@ieakenya.or.ke**
Wavuti: **http://www.ieakenya.or.ke**

## Sanduku 1: Ratiba ya bajeti katika serikali ya kaunti na kitaifa.

**Augosti 30.** Hazina ya kitaifa hutoa taarifa kwa mashirika ya kiserikali na kuanzisha harakati

ya bajeti na kushirikisha umma kwa kufuata muongozo maalum. Afisa mkuu wa fedha katika kaunti lazima pia asambaze taarifa kufikia tarehe hii vilevile katika kaunti.

**Septemba 1.** Kaunti lazima watayarishe na kuwasilisha taarifa ya mipangilio ya miradi ya maendeleo katika bunge la serikali ya kaunti kufikia tarehe hii. Mpangilio huo husambazwa kwa umma katika siku 7.

**Septemba 1 hadi Februari 15.** Wakati huu hazina ya kitaifa na baadhi ya wizara na mashirika ya serikali hujadiliana na umma na wadau. Aidha vikao pia vya umma huandaliwa na maoni yao kujumuishwa katika mapendekezo ya bajeti.

**January 1.** Kufikia mwezi Januari kila mwaka tume ya mgao wa mapato ya kitaifa CRA hutoa mapendekezo yake kwa serikali ya kaunti na ya kitaifa.

**Februari 15.** Waziri wa fedha hutoa taarifa ya sera ya bajeti wakati huu. Kadhalika ndiyo tarehe ya mwisho ya kuwasilisha taarifa ya mikakati ya kudhibiti mikopo na mswada wa mgao wa mapato kwa serikali ya kaunti bungeni.

**Februari 28.** Tarehe ya mwisho ya kuidhinisha taarifa ya sera za bajeti bungeni. Hii ndiyo tarehe ya mwisho pia ya kuwasilisha taarifa kuhusu mikakati ya kifedha katika serikali za kaunti.

**Machi 1.** Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha taarifa ya sera za bajeti kwa umma.

**Machi 16.** Hii ndiyo tarehe ya mwisho ya kupitisha mswada wa mgao wa mapato ya kitaifa katika kaunti

**Aprili 30.** Hii nidyo tarehe ya mwisho kwa waziri wa fedha kuwasilisha makadirio ya bajeti bungeni. Ni tarehe ya mwisho pia kwa idara ya mahakama na tume ya huduma za bunge kutoa bajeti yao pia bungeni. Mapendekezo ya bajeti ya kaunti pia huwasilishwa wakati huu

**Mei.** Huu ndio wakati kamati ya bunge kuhusu fedha na bajeti hufanya vikao vya umma kukusanya maoni .

**Mei-Juni.** Hii ndiyo tarehe ambapo kamati ya bunge kuhusu fedha na bajeti hutoa mapendekezo yao bungeni.

**Mei 15.** Hii ndiyo siku ya mwisho ambapo waziri wa fedha hutoa maoni yake kuhusu makadirio ya bajeti ya idara ya mahakama na bunge.

**Juni.** Mswada wa kitaifa wa fedha unaoidhinisha kukusanya ushuru huwasilishwa bungeni. Mswada wa fedha wa kaunti pia huwasilishwa katika bunge la kaunti

**Juni 30.** Huu ndiyo mwisho wa mwaka wa kifedha kwa mswada wa matumizi ya fedha kupitishwa na bunge ili kuidhinisha matumizi ya fedha za bajeti ya mwaka mpya.

**Julai.** Katika mwezi huu makadirio ya bajeti yalipitishwa husambazwa kwa umma

**Novemba.** Serikali lazima ichapishe mtazamo wa bajeti ili ikaguliwe na kutofautisha utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita na mitzamo wa bajeti kutoka kwa taarifa ya sera za bajeti mwezi Februari. Hatahivyo mtizamo wa bajeti ya kaunti hauna tarehe ya mwisho kuwasilishwa katika bunge la kaunti lakini itayarishwe katika wakati huu.

**Desemba 15.** Serikali inapaswa kuchapisha ripoti na kutekelezwa katika miezi mitatu ya kwanza katika mwaka wa kifedha kuanzia Julai hadi Septemba kabla siku 45 baada ya robo ya kwanza ya mwaka wa kifedha kuisha.

## Tafsiri

**Maafisa wa uhasibu.** Kila shirika la serikali lazima liwe na mhasibu. Afisa huyu huteuliwa na waziri wa fedha au afisa mkuu wa fedha katika kaunti.Afisa huyu ana jukumu la kusimamia fedha za shirika na kutoa ripoti. Maafisa hawa hutakiwa kuwajibika ikiwa kutakuwa na ufujaji wa fedha.

**Mswada wa matumizi ya fedha.** Mswada huu lazima uidhinishwe na bunge ili kuwezesha matumizi ya fedha za bajeti. Ndiyo idhini maalum ya kuipa ruhusa serikali kutumia fedha za bajeti. Serikali ya kaunti pia hupitisha mswada huu kuwezesha matumizi ya bajeti ya kaunti.

**Makadirio ya bajeti.** Haya ni mapendekezo ya bajeti yanayowasilishwa bungeni Aprili 30. Mapendekezo haya ya bajeti huweka wazi matumizi ya fedha ya wizara zote yanayojumuisha matumizi ya fedha ya kawaida na ya maendeleo.

**Taarifa ya sera ya bajeti (BPS)** Huu ni waraka rasmi unaotolewa na serikali inayonakili mipango ya bajeti ya mwaka ujao. Hujumuisha majadiliano ya mienendo ya kiuchumi na mtazamo wa matumizi na mapato ya serikali. Taarifa ya BPS inapaswa kuwasilishwa bungeni katikati ya mwezi wa Februari na kusambazwa kwa umma mwisho wa mwezi wa Februari.

**Taarifa ya ukakuguzi na mtizamo wa bajeti. (BROP).** Ripoti hiyo hutolewa kila mwaka katika mwezi Septemba na kuchapishwa mwezi Novemba.Taarifa hii hukagua utendakazi wa serikali katika mapato na matumizi ya fedha na ikiwa walifikia malengo yao mwaka uliopita. Taarifa hiyo hutoa mtizamo wa mwaka uliopo uliyoangaziwa katika taarifa ya sera za bajeti.

**Waziri wa fedha.**Katika mfumo wa uongozi wa sasa waziri huteuliwa kutoka nje ya bunge tofauti na mfumo wa awali

**Hazina ya dharura na ustawi wa maendeleo.** Hii ni hazina maalum iliyotengwa kushughulikia mikasa ambayo haikupangiwa

wakati bajeti ikipangwa. Fedha hizo zitumike kukabiliana na hali za dharura zinazoweza kuathiri watu na maslahi yao.

**Msimamizi wa Bajeti.** Mwenye cheo hiki huhakikisha serikali inafuatilia na kuhakikisha uwajibikaji na uwazi katika utendakazi serikalini. Msimamizi wa bajeti huhakikisha fedha zimetumika kwa njia iliyo halali na huandika ripoti kuhusu utekelzaji wa sera.

**Mswada wa mgao wa fedha za kaunti.** Mswada huu unapaswa kuwasilishwa bungeni ili kutoa mwongozo wa kiwango cha fedha kinachotolewa katika kaunti 47. Idadi ya kaunti imetajwa katika mswada wa mgao wa mapato. Tume ya kitaifa ya mgao wa mapato imependekeza kwamba mapato yagawanywe kupitia taratibu maalum itakayoangaziwa katika mswada wa mgao wa mapato ya kaunti.

**Jukwaa la kujadili bajeti na uchumi katika kaunti.**Jukwaa hili hutumiwa kufanya majadiliano kuhusu mipango na bajeti katika serikali ya kaunti. Hujumuisha wanachama kutoka sekta mbalimbali Hazina ya fedha za dharura na ustawishaji wa maendeleo. Hazina hii ya kaunti inafanana na hazina ya kitaifa ya dharura na hufuata masharti hayohayo.

**Afisa mkuu wa fedha katika kaunti.** Cheo hiki ni sawiya na kile cha waziri wa fedha tofauti ni serikali ya kaunti.

**Taarifa ya mikakati ya fedha.**Taarifa hii ni Bunge la kitaifa. Ni mojawapo ya bunge chini sawia na ile taarifa ya kitaifa ya sera za bajeti.

**Wizara ya fedha ya kaunti.** Wizara ya fedha ya kaunti hujumuisha afisa mkuu wa fedha, afisa mkuu mtendaji wa fedha na idara zinazohusika na maswala ya fedha.

**Mswada wa mgao wa mapato.** Mswada huu huwasilishwa bungeni ili kuangazia kiwango gani cha mapato ya kitaifa kitagawanywa kwa serikali ya kitaifa na serikali ya kaunti. Baada ya hatua hii kuafikiwa mswada huo huelekeza kiwango gani kitasambazwa kwa kila kaunti.

**Mswada wa Fedha.** Mswada huu huwasilishwa bungeni kuidhinisha vigezo vya ushuru na mapato. Humu nchini Kenya mswada huu hupitishwa kando na makadirio ya bajeti. Katika serikali ya kaunti, lazima pia uidhinishwe na bunge la kaunti ili waweze kukusanya ushuru na mapato.

**Baraza la taasisi za serikali kuhusu bajeti na uchumi.** Baraza hili hujumuisha waziri wa fedha na maafisa wakuu wa serikali ya kaunti wa fedha ili kujadili maswala yanayowaathiri katika ngazi ya kaunti na kitaifa.

**Bunge la kitaifa.** Ni mojawapo ya bunge chini sawia ya katiba mpya inayojumuisha bunge la kitaifa la wabunge waliochaguliwa kutoka maeneo bunge. Seneti inajumuisha wawakilishi kutoka kaunti zote.

**Wizara ya fedha.** Wizara ya fedha inajumuisha waziri wa fedha, katibu mtendaji wa fedha na idara zinazohusika na maswala ya uchumi

**Afisi ya bajeti bungeni.** Ofisi hii ina jukumu la kufanya utafiti na kuimarisha jukumu la bunge la bajeti na kamati ya bunge kuhusu bajeti na fedha. Afisi hii hufanya tathmini ya bajeti inayowezesha wabunge kuelewa bajeti inayowasilishwa kwao kila mwaka na idara mbalimbali za serikali.

**Seneti.** Mojawapo ya mabunge .Tazama tafsiri ya bunge la kitaifa

**Bajeti ya ziada.** Bajeti ya ziada hupitishwa kila mwaka wa kifedha baada ya kuidhinishwa na bunge. Bajeti hii huletwa bungeni kutokana na mapungufu katika makadirio ya bajeti rasmi au mahitaji ya serikali ambayo hayakupangiwa sawasawa.Bajeti ya ziada hupangwa kwa asilimia 10 ya bajeti rasmi ya kitaifa. Bunge huidhinisha kiwango cha juu ya asilimia 10% wakati ambapo kuna sababu kuu na iliyo maalum.

1. Inakisiwa kwamba bunge lina hadi Juni 30 kupitisha bajeti na hivyo basi kusalia na miezi 2 kuijadili na kufanya marekebisho. Kwa kawaida, tayari kamati ya bunge huwa wameshafanya vikao vyao mwezi Mei ambapo hupokea maoni hii ni kwasababu katiba imeweka mipaka kuhusu kiwango cha marekebisho yanayoweza kuwasilishwa kwa kamati ya bunge kuhusu bajeti.
2. Sheria ya PFM, 25:6; 10:2. 3. Sheria ya PFM 35:2.
4. Majukumu haya yameandikwa katika ratiba ya nne ya katiba.
5. Tazama wizara ya fedha"Mashauriano ya wadau wa kaunti" 2012/13-2014/15 Bajeti ya MTEF," November 2011.
6. Mwaka huu,kikao kilifanywa Oktoba 30 katika mahakama ya Milimani
7. Sheria ya PFM, 36:2. 8. Sheria ya PFM, 207.
9. Sheria ya PFM, 37
10. Sheria ya PFM, 37:8.
11. Sheria ya PFM, 39:3.
12. Katiba, 114. Mswada wa fedha hujumuisha mapendekezo ya makadirio ya bajeti.
13. Sheria ya PFM, 39:5.
14. Sheria ya PFM, 83:5.
15. Sheria ya PFM, 26.
16. Sheria ya PFM, 39:8.
17. Sheria ya PFM, 27.
18. Sheria ya PFM, 15:2.
19. Sheria ya PFM, 33.
20. Sheria ya PFM, 31.
21. Sheria ya PFM, 62-64.
22. Sheria ya PFM, 43:2.
23. Katiba, 223.
24. Sheria ya PFM, 20-21.
25. Katiba, 216
26. Katiba, 204. 27. Katiba, 216.
28. Sheria ya PFM , 190.
29. Katiba, 217.
30. Kuelewa utaratibu,tazama www.crakenya.org
31. Katiba, 218:1.
32. Sheria ya PFM, 42.
33. Sheria ya PFM, 17:6
34. Sheria ya PFM, 94.
35. Sheria ya PFM, 97:2-4.
36. Sheria ya PFM, 99.
37. Sheria ya PFM, 117.
38. Sheria ya PFM, 117:6, 117:8.
39. Sheria ya PFM, 128:2.
40. Sheria ya PFM, 129:2a.
41. Sheria ya PFM, 131:2.
42. Sheria ya serikali za kaunti, 21.
43. Sheria ya PFM, 131:3.
44. Sheria ya PFM, 107.
45. Sheria ya PFM, 110-114.
46. Sheria ya PFM, 135.
47. Sheria ya PFM, 154:2.
48. Sheria ya PFM, 134.
49. Sheria ya PFM, 131:5.

50. Sheria ya PFM, 166.
51. Sheria ya PFM, 118.
52. Sheria ya PFM, 123.
53. Sheria ya PFM, 122:5.
54. Katiba, 212.
55. Sheria ya PFM, 138.
56. Katiba, 209.
57. Sheria ya PFM, 40:3.
58. Sheria ya PFM , 43.
59. Sheria ya PFM, 46:2.
60. Sheria ya PFM , 133.
61. Sheria ya PFM, 67.
62. Sheria ya PFM, 148.
63. Sheria ya PFM , 68:1b.
64. Sheria ya PFM 68: 2f.
65. Sheria ya PFM 68:3.
66. Sheria ya PFM, 74.
67. Sheria ya PFM, 73.
68. Sheria ya PFM, 68:2k.
69. Sheria ya PFM, 196-99, 202.
70. Sheria ya PFM, 204.
71. Sheria ya PFM, 173.
72. Sheria ya PFM, 175:8.
73. http://cickenya.org/bills/urban-areas-and-cities-act-2011
74. Sheria ya PFM, 175:9.
75. Sheria ya PFM, 170.\
76. Sheria ya PFM , 177.
77. Sheria ya PFM, 178.
78. PFM Act, 5. Mashauriano ya swala hili kwa muktadha wa rasilmali ya maji"Ugatuzi bila matatizo": Mchakato wa Kenya mpya""' October 2012, Sura ya 7.
79. Katiba, 227.
80. http://www.kenyalaw.org/klr/fileadmin/ pdfdownloads/Acts/_Cap412C_.pdf (Sheria ya kudhibiti zabuni na mauzo ya serikali)

Commission for the Implementation of the Constitution
Utekelezaji wa katiba, jukumu la wote

IBP | KENYA
Open Budgets. Transform Lives.